

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**Kikao cha Thelathini na Nane – Tarehe 28 Mei, 2018**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Dkt Tulia Ackson ) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

**NDG. ASIA MINJA - KATIBU MEZANI:**

**TAARIFA YA SPIKA**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, taarifa ya Spika kwa mujibu wa Kanuni ya 33(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za mwaka 2016.

Waheshimiwa Wabunge, kwa masikitiko makubwa, Mheshimiwa Spika anapenda kuwajulisha kuwa Bunge letu limepatwa na msiba mkubwa wa kuondokewa na Mheshimiwa Mwalimu Kasuku Samson Bilago, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Buyungu. Mheshimiwa Bilago alifariki Jumamosi tarehe 26 Mei, 2018 katika Hospital ya Taifa ya Muhimbili alikokuwa akipatiwa matibabu. Kabla ya kupelekwa Muhimbili marehemu alipata matibabu katika Hospital ya *DCMC* iliyoko eneo la Ntyuka, Jijini Dodoma na tarehe 22 Mei, 2018 ndipo alipohamishiwa Muhimbili kwa ajili ya matibabu zaidi.

Waheshimiwa Wabunge, kufuatia msiba huo, taratibu mbalimbali zimeendelea kufanyika kati ya Ofisi ya Bunge,

familia ya marehemu na Chama cha Demokrasia na Maendeleo. Mpaka sasa tumefikia hatua ifuatayo:-

(a) Mwili wa marehemu utaletwa hapa Bungeni siku ya Jumanne tarehe 29 Mei, 2018 ili Waheshimiwa Wabunge mpate fursa ya kutoa heshima za mwisho.

(b) Baada ya zoezi la kuaga mwili wa marehemu kukamilika, mwili utasafirishwa siku hiyo ya Jumanne yaani kesho kwenda Kijiji cha Kasuga, Wilaya ya Kakonko, Mkoani Kigoma, ambapo mazishi yanatarajiwa kufanyika siku ya Jumatano tarehe 30 Mei, 2018. Katika mazishi hayo Bunge letu litawakilishwa na:-

- (1) Mheshimiwa Spika;
  - (2) Katibu wa Bunge;
  - (3) Wawakilishi wa Wajumbe wa Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii;
  - (4) Wabunge wote toka Mkoa wa Kigoma;
  - (5) Mwakilishi wa Wabunge kutoka Zanzibar;
  - (6) Wawakilishi wa Wabunge kutoka vyama vyote vyenye uwakilishi Bungeni;
  - (7) Wawakilishi wa Tume ya Utumishi wa Bunge;
- na
- (8) Wabunge wengine watakaochaguliwa.

Waheshimiwa Wabunge, inatarajiwa kuwa Wabunge watakaokwenda kutuwakilisha kwenye mazishi hayo wataondoka Dodoma siku ya Jumanne asubuhi na kurudi Dodoma siku ya Jumatano mara baada ya mazishi.

Waheshimiwa Wabunge, kufuatia tukio hilo kwa mujibu wa Kanuni ya 33(2) ya Kanuni zetu za Bunge siku ya leo hatutaendelea na kikao cha Bunge badala yake tutakuwa na maombolezo ya msiba wa mwenzetu. Aidha, siku ya kesho Jumanne tarehe 29 Mei, 2018 tutakuwa na Kikao cha Bunge kama kawaida isipokuwa tutaahirisha Bunge saa sita mchana, ili kutoa fursa kwa shughuli za kutoa heshima za mwisho kwa mwili wa marehemu Mheshimiwa Bilago. Baada

ya hapo, tutaendelea na maombolezo hadi siku ya Jumatano ambapo Bunge litaendelea.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya taarifa hiyo, sasa naomba tusimame kwa muda wa dakika moja kama ishara ya kuomboleza kifo cha mwenzetu.

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge  
walisimama kwa muda wa dakika moja)*

**NAIBU SPIKA:** Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi, amina.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 3.10 Asubuhi Bunge Liliahirishwa mpaka Siku ya  
Jumanne, Tarehe 29 Mei, 2018, Saa Tatu Asubuhi)*